Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Dhima Katika Mawasiliano ya Ushairi wa Jando Katika Jamii ya Watachoni, Kaunti ya Bungoma

**Richard Makhakha Iyaya[1]; Prof. Nabea Wendo[2]; Dkt. Gwachi J. Mayaka[3]**

**[1,2,3] Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya**

**Main Author Email: richard.iyaya@gmail.com**

## IKISIRI

Makala haya yalilenga kuchunguza dhima ya mawasiliano ya ushairi wa jando kwenye jamii ya Watachoni wa kaunti ya Bungoma. Utafiti uliendelezwa kwa muundo wa kimaelezo ya kiethnografia ulioangazia kanuni za mila, utamaduni na mahusiano ya kimawasiliano na athari zake kwa mitindo na lugha ya uwasilishaji ili kubainisha dhima yake. Nadharia ya Baada ya Umuundo ya Derrida (1966) ilitumika kuchanganua miundo na kuonyesha kuwa matini hubainisha ukinzani wa ujumbe anaouhusisha mwasilishaji katika kazi yake. Nadharia ya ubabe-dume ya Maclennes (1998) pia ilitumika kuchunguza namna mitindo ya uwasilishaji na lugha katika mawasiliano ya ushairi wa jando unavyoathiri asasi za kijamii. Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji wa deta moja kwa moja kutoka jamii ya Watachoni wakati wa shughuli za jando kwenye Kaunti ya Bungoma. Kundi lengwa lilikuwa watahiriwa, wazazi, wanaume na wanawake Watachoni na viongozi wa shughuli za jando. Tulitumia sampuli kusudio na sampuli nasibu tabakishi kubainisha ushairi na wasailiwa waliorejelewa kuyaainisha mawasiliano haya ya ushairi wa jando. Ushairi 16 na watafitiwa 45 walirejelewa kuyachanganua mawasiliano haya katika awamu zote za shughuli za jando. Deta iliyokusanywa ilirekodiwa, ikaandikwa na kutafsiriwa kutoka lugha ya Kitachoni hadi ya Kiswahili kisha ikachanganuliwa. Utafiti huu ulitumia mbinu za uchunguzaji nyanjani, mahojiano, mashauriano na wasimamizi na kuainisha habari zilizotokana na vyombo vya habari. Vifaa kama vile kamera za picha tuli na za kunasa sauti na video vilitumika kukusanyia deta na hatimaye kuziwasilisha kwa njia za maelezo na majedwali. Deta iliwasilishwa kwa njia ya maelezo na kufafanuliwa kwa kuzingatia malengo, nadharia na mipaka ya utafiti.

**Maneno muhimu:** Dhima, umuundo, ubabe-dume, jando, watahiriwa, majukumu, mawasiliano.

-------------------------------------------------------------------***-------------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Iyaya R.M, Nabea, W., & Mayaka, G. J. (2020). Dhima katika mawasiliano ya ushairi wa jando katika jamii ya watachoni, kaunti ya Bungoma. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 98-109.

-------------------------------------------------------------------***-------------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## Utangulizi

Mawasiliano ya ushairi wa jando ni shughuli muhimu inayotumika katika jamii ya Watachoni kupitisha mafunzo muhimu kuwatayarisha wavulana wao wanaobalekhe kwa majukumu muhimu ya utu uzima wao. Mawasiliano haya huwasilishwa kwa mitindo na lugha teule kupitia katika ushairi wa jando na kuibua maudhui muhimu ili kuafiki dhima zake mbalimbali. Kupitia mawasiliano haya, wanajamii wa jinsia, umri na staha tofauti katika jamii hubainisha majukumu yao ya kibinafsi, kifamilia na kijamii. Ili mawasiliano haya yaweze kueleweka inavyostahili kwa watahiriwa walengwa kuandaliwa kwa majukumu muhimu yanayolengwa kuyatekelezwa kulingana na mila ya Watachoni, dhima ya mawasiliano haya yafaa ieleweke.

Lakini, lugha katika ushairi huu imekumbwa na sintofahamu kubwa na ugumu wa kuitafakari inapotumika wakati wa hii tohara. Vilevile, suala la dhima inayojitokeza katika mawasiliano haya halijatambulika na kutiliwa maanani kupitia utafiti wa kiakademia. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza dhima inayojitokeza katika mawasiliano ya ushairi wa jando na namna inavyofanikisha shughuli za jando katika jamii ya Watachoni wa Kaunti ya Bungoma. Ijapokuwa suala la kuchunguza dhima, maudhui na matumizi ya lugha limeshughulikiwa katika tafiti zingine za awali, hakuna hata moja ambayo imefanywa katika mawasiliano ya ushairi katika jamii ya Watachoni. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili kwa kuhakiki kwa kina mawasiliano ya ushairi wa jando na umuhimu wake katika jamii ya Watachoni wa Kaunti ya Bungoma kwa kuhakiki dhima.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Ushairi katika jamii nyingi za zamani na haukuandikwa kutokana na wanajamii kutojua kusoma na kuandika nyakati hizo. Uchunguzi uliofanywa ulidhibitisha kuwa asili ya ushairi simulizi ni nyimbo zilizoimbwa tangu awali kwa dhima maalumu japo hazikufuata utaratibu maalumu. Ingawa ziliimbwa kwa lugha za kienyeji, zilitumia lugha nzito ambayo haikuwa ya kawaida na iliyosheheni hekima (Musira, 2015). Walioimba nyimbo hizi katika sherehe zozote hawakuimbwa ovyo bali walifuata kanuni bainifu kwa muktadha wa sherehe husika hivyo ushairi wa jando haungeimbwa harusini hali kadhalika kwenye mazishi na hukidhi dhima ileile moja. Tanzu za fasihi simulizi husheheni dhima nyingi kwenye jamii mathalani kufunza maadili na kuendeleza historia za jamii husika. Wanajamii hufundishwa mambo mengi hasa masuala ya utu uzima, mapenzi na ndoa, nasaha kwa jamii, kuliwaza na kukemea matendo kwa hivyo kuwa na mchango mkubwa mno katika jamii yoyote ile.

Kwa muda sasa, ushairi umekuwa ukitumika kukidhi mahitaji ya jamii za kilimwengu. Ukweli huu ulibainika katika kazi mbalimbali za kilimwengu hivyo kudhihirisha uwezekano wa kuwa vivyo hivyo katika jamii za Kiafrika ikiwemo ya Watachoni. Katika maeneo ya Antaktika, makala ya (Leane, 2015) yaliyochapishwa katika Kiingereza yalikuwa yenye mchango mkubwa katika jamii hii. Tangu yachapishwe, maeneo ya Antaktika pamoja na Southern Ocean yalichochea mchakato wa utoaji wa "mashairi toshelezi yaliyokidhi mahitaji ya idadi ya umma (Truswell, 2014). Mafungu ya makala na ushairi wa Antaktika yalikuwa na mawanda mapana kama vile masimulizi marefu ya kiepiki, tungo fupi, hadithi za



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kishujaa ,sanaa za umbuji na ulimbwende na tafiti za kimaisha. Tafiti hizi zilidhihirisha kuwa ushairi ulikuwa na dhima kuu katika kuangazia maisha kwenye jamii za kilimwengu. Ugunduzi katika utafiti huo ulituelekeza kuchunguza mawasiliano ya ushairi wa jando na tukapata kuwa unachangia sana katika ujenzi wa maadili ya kijamii. Vilevile, mawasiliano haya yaliendeleza kuhifadhi utamaduni na historia ya jamii ya Watachoni kwa kuwaandaa watoto wao kwa majukumu ya kudumisha katika utu uzima wao.

Ushairi kama kipengele cha fasihi umewekwa katikati ya fasihi halisia na dhahania. Uelewa na dhima yake hutegemea muktadha wa uwasilishwaji na lugha inayotumika kwenye uwasilisho wake. Gill na Waters, (2009) walikubaliana na usemi huu waliposema kuwa ushairi mahususi huweza kuzua hali ya kifikra, kitawasifu, au tafakuri fulani za matini hasa kuhusu watu na mazingira yao. Katika kazi ya Leane ya *Antarctica in Fiction* (2012) yaliyochukuliwa kuwa yenye umakini wa kina kuhusu fasihi ya Antaktika, mtunzi huyu alitofautisha kati ya dhahania lengwa kupitia masimulizi ikiwemo tenzi za mashairi na ile fupi ya mashairi ya Kiantaktika. Hali hii ilidhihirisha kuwa ushairi husaidia kuumba na kuumbua jamii katika miktadha ya shughuli mbalimbali. Utafiti huo ulitusaidia kubainisha namna mawasiliano ya ushairi wa jando pia huwa muhimu katika ujenzi wa maadili yanayoendeleza utamaduni na historia thabiti kutokana na mafunzo ya jando wanayopewa watahiriwa.

Ushairi hudumisha siri na tamaduni za jamii. Kulingana na M'ngaruthi (2008), lugha na mitindo ya uwasilishaji hueleweka na wale waliopitia shughuli husika kwani ujumbe unaopitishwa hueleweka tu na waliopitia kulingana na dhima yake. Abu-Lughod (1986) katika utafiti wake, alichunguza mashairi yaliyokuwa yanaimbwa na wanawake wa Kibedouin katika muktadha na mazingira ya siri kubwa ili matini yake yasijulikane kwa wanaume. Mashairi hayo yalilenga kusambaza mafunzo kwa wanawake waweze kupambana kupinga ukandamizwaji waliofanyiwa na wanaume. Ukandamizaji huo ulipigiwa chapuo kwa mashairi yaliyoimbwa yakilenga kuwahimiza wanawake wawe watiifu kwa waume wao. Mashairi yaliyoimbwa na wanawake wa kabila hili yakitumia msamiati ulioashiria heshima, mamlaka na chuki ya kutawaliwa na kunyanyaswa na wanaume. Sawa na utafiti wa Abu-Lghod, mawasiliano ya ushairi wa jando yalilenga walioshiriki na walioshirikishwa pekee yao. Ujumbe ulilenga jamii siri ya Watachoni kuwasilisha mambo kimkutadha na kwa upekee ili walelengwa pekee wauelewe katika mikutadha dhamirivu. Kulingana na Lihraw (2010), jamii ya Watachoni ilikuwa ya watu waliokuwa na falsafa iliyofichika na kufanya uelewa wake kuonekana tata kwa watahiriwa na jamii jirani. Uelewa huu ulituongoza katika kubainisha dhima katika haya mawasiliano ya ushairi wa jando kwa kujikita katika malengo, upeo na mihimili ya nadharia zilizouongoza utafiti huu.

Coplan (1987) katika utafiti wake alibaini kuwa wanawake wa Lesotho walipinga kunyanyaswa na wanaume kwa kutumia mashairi. Mantiki ya kutambua tofauti za kiitikadi kwa kuzingatia jinsia ilisababisha kuwepo kwa mijadala ya kiitikadi kuhusu tofauti kati ya wanawake wenyewe. Ilibainisha tofauti baina ya wanaume na wanawake kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi zilizokuwa pamoja na



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ushairi. Tulichojifunza kutokana na utafiti wa Coplan (keshatajwa) ilikuwa kwamba wanawake walitofautiana kuufasili ulimwengu kutokana na nafasi yao katika jamii. Matokeo ya utafiti huu wa Coplan ulituelekeza kuchunguza namna mawasiliano ya ushairi wa jando yalivyotumika kupanga migao ya majukumu katika jamii ya Watachoni. Kwa mfano, mihimili ya nadharia ya Ubabe - dume ilitujuza namna wanaume hupewa majukumu kutokana na mawasiliano ya ushairi wa jando yanayowaweka juu ya wanawake na jamii nzima.

Katika jamii nyingi za Kiafrika, ushairi ulitumiwa kuvitayarisha vizazi vyake kwa majukumu ya baadaye ya kifamilia na kijamii. Alembi (1991) aliunga mkono kauli hii kwa kudhihirisha kuwepo usawiri wa mahusiano ya kijinsia katika ushairi wa michezo ya watoto katika jamii nyingi za Kiafrika. Alitumia mfano wa ushairi wa watoto katika jamii ya Wamaragoli ambapo watoto walibebana migongoni wakiimba mashairi huku aliyebebwa akiuliza maswali kuhuhu alikokuwa akipelekwa. Mbebwa alielezwa kuwa alikuwa akipelekwa kwa wakwe zake kwani alikuwa ameshaolewa. Ujinsia ulijitokeza waziwazi katika ushairi huo wa watoto Wamaragoli kwani wasichana waliandaliwa kwa kutumia ushairi huu wa michezo ya watoto kuwa siku moja wangeozwa na wazazi wao ili wapewe mahari ya ng'ombe, mbuzi au kondoo wanane. Kwa ufahamu huo, mawasiliano ya ushairi wa jando ulilenga kutoa mafunzo kwa watahiriwa kwa lengo ya kuwaandaa kwa majukumu yao ya utu uzima katika jamii. Jambo hili lilitudhihirishia kuwa wanawake hawakuwa na uhuru wa kufanya maamuzi ilivyojitokeza katika utafiti wa Alembi vilevile katika mawasiliano ya ushairi wa jando. Ilikuwa dhahiri kuwa wanawake wamepewa nafasi ya kujalizia na kukamilisha hadhi ya mwanamume katika jamii nyingi za Kiafrika. M'ngaruthi (2008) alisema kuwa tamasha za utamaduni ziliwaandaa viongozi kwani ziliwatayarisha kuwa wasemaji mashuhuri waliokuwa na maadili mema kupitia mafunzo ya tohara mbalimbali.

Ushairi huakisi hali na majukumu ya wanajamii mbalimbali katika jamii. Ukweli wa kauli hii umethibitika katika utafiti wa Salem (2013) alioufanya kuhusu usawiri wa jinsia katika lugha ya mashairi ya Shabaan Robert kwenye vitabu vya Pambo la Lugha na Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini. Ilibainika kuwa tamathali za semi zilitumika kusawiri masuala ya kijinsia katika mashairi hayo na kueleza mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume kupitia tamathali za semi hizo zilitumika kumchora mwanamke tofauti na jinsi zilivyotumika kumchora mwanaume kupitia ushairi. Utafiti huo wake ulifanana na wetu kwa vile ulikuwa umechanganua kipengele cha mashairi katika kazi ya Shabaan Robert huku wetu ukiangazia ushairi katika mawasiliano ya jando kwenye jamii bainifu ya Watachoni. Hata hivyo, ulitufaa katika kuangazia dhima iliyorejelea nafasi ya mwanamke na mwanamume katika jamii ilivyojitokeza katika mawasiliano haya huku tukiongozwa kwa nadharia ya baada ya umuundo na nadharia ya ubabe-dume kama zilivyotumika katika utafiti huu.

Katika jamii ilivyo ya Waswahili, alibainika kuwa na serana itikadi zilizohalalisha ukiritimba wa wanaume ulioegemezwa kwenye matumizi ya kaida za kitamaduni, dini na tofauti za kijinsia. Kauli hii iliungwa mkono na Momanyi (2007) kuwa tofauti za kijinsia hudhihirika



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

katika Tanzu za fasihi kama vile ushairi zilipotafitiwa. Kwa muda mrefu, utamaduni ulisemekana kuwapa wanaume wa jamii ya Waswahili mamlaka ya kuwatawala wanawake kupitia mfumo dume. Kimsingi, tofauti hizi zilitumika kwa hila za utamaduni wa jamii zilizowatetea wanaume kama jinsia yenye mamlaka juu ya Wanawake. Kilichoonekana katika jamii mbalimbali kilikuwa kwamba nafasi ya wanawake ilikuwa ni kuunga mkono itikadi za wanaume na kuiamilia hali hii. Kitu kilichovutia zaidi ni kwamba hali hiyo ilikuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku kwenye jamii mbalimbali za Kiafrika na haikudhihirika hadi iwekwe peupe kupitia matokeo ya kiutafiti. Momanyi alisema kuwa jamii ya Waswahili ilikuwa ikitumia vipengele na miundo ya kifasihi kutetea u-ume ili kuilinda na kuendeleza nafasi kandamizi ya wanaume. Ugunduzi huo wa Momanyi ulituongoza kuchunguza namna mawasiliano ya ushairi wa jando yanavyohalalisha ubabe - dume katika jamii ya Watachoni.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili. Nadharia ya baada ya umuundo ya Jacques Derrida (1966) ilitumika kuonyesha kuwa matini yote huwa na maana tatanishi na misamiati haiwi na maana dhahiri hivyo huweza kuwa na tafsili nyingi zisizo kikomo. Hivyo basi, aina ya mitindo ya uwasilishaji katika sanaa yoyote hutegemea ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa kama dhima. Sanaa ya ushairi katika mawasiliano ya jando hulenga kutimiza malengo muhimu ya kuwafunza watahiriwa mila za Watachoni ili wafuzu kuchukua majukumu ya utu uzima. Hivyo basi, nadharia hii ilituelekeza kubainisha namna jamii inavyopitisha mafunzo kupitia tohara za jando na kuathiri miundo ya maisha katika jamii ya Watachoni. Katika kubainisha mitindo na lugha inayotumika na wawasilishaji, mihimili ya nadharia hii ilizingatiwa kubainisha dhana ya nafsi inayotumika na mtunzi kuwasilisha ujumbe unaolenga kuathiri hadhira yake. Mihimili ya nadharia hii iliongoza kubainisha maana kusudiwa na maana kamili inaokusudiwa katika mitindo ya uwasilishaji katika mawasiliano haya ya ushairi wa jando ya Watachoni.

Nadharia ya Ubabe-dume iliyoasisiwa na Maclennes (1998) pia ilitumika kubainisha nguvu za mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume hasa kutokana na asasi za kijamii husika. Pia inabainisha masharti ya kihistoria na kitamaduni yanavyohalalisha mielekeo na mitazamo tofauti baina ya jinsia ya kike na ya kiume katika misingi ya kubainisha dhima ya haya mawasiliano katika jamii. Maclennes anaeleza kuwa udume hauwezi kubainishwa kama sifa ya mwanamme bali hutokana na itikadi za kitamaduni ambazo ndizo huzaa mielekeo na matarajio ya utamaduni wa jamii husika. Baadhi ya rai katika mawasiliano huweza kusababisha mielekeo kwamba mwanamme huwa na mamlaka yote juu ya mwanamke kwa aghalabu hali zote za maisha. Nadharia hizi mbili ziliongoza katika kuhakiki dhima zilizolengwa kubainishwa kwa mitindo ya uwasilishwaji na matini katika mawasiliano ya ushairi huu inayodhihirisha kupitia mihimili yake ya nguvu na udhabiti, ujasiri, umilisi na umahiri na heshima na maadili. Nguzo hizi zilitumika kubainisha malengo ya aina ya lugha na ujumbe uliotolewa kwa watahiriwa na viongozi wa shughuli za jando katika hatua zote tatu: matayarisho, kupitia kuingia hadi kutoka jandoni.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**MATOKEO**

**Dhima ya Kudumisha Utamaduni na Kuendeleza Historia ya Jamii**

Katika kuhifadhi amali muhimu za kijamii, fasihi simulizi huwa nyenzo muhimu. Aidha, wanajamii hufahamishwa kupitia fasihi simulizi kuwa wao ni nani na wanachimbukia wapi. Maarifa haya huwa muhimu kwa kila mwanajamii kwani humsaidia siyo tu kujielewa bali pia kujitambua. Mawasiliano ya ushairi wa jando ni kipengele cha fasihi simulizi hivyo basi huambatanishwa na desturi mbalimbali za jamii husika ambazo aghalabu hutofautisha jamii moja hadi nyingine. Mawasiliano haya yalilenga kuwatambulisha Watachoni pamoja na desturi zao na kubainisha kaida , mila na desturi za jamii yao kwa kuzipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia shughuli na mafunzo ya jando. Mafunzo yanayotolewa kwao kuhusu majukumu ya utu uzima kama inavyojitokeza katika ushairi MMSJ 5 yalilenga kudumisha utamaduni na Kuendeleza historia ya Watachoni. Ushairi wa MMSJ 4 unabainisha namna ngariba anavyowapa watahiriwa ushauri dhidi ya kushinda katika vyumba vya wazazi hasa anacholala mamake na jikoni wakati wote. Vilevile anamshauri dhidi ya kuwa mzinzi hasa kwa wanawake wa wenyewe kwani ni hatari hata ya kuleta mauti. Katika ushairi wa MMSJ 3, babu anamuuliza mtahiriwa aliye mjukuu wake kuendeleza mila ya jando iliyoanza siku nyingi zilizopita na kuiadhimisha kishujaa. Ushairi wa MMSJ 6 unamtaka mtahiriwa kuendeleza desturi ya maadili ya kijamii yaliyo sehemu ya utamaduni na historia ya Watachoni.

Ushairi wa MWSJ 6, MWSJ 3, MWSJ 7, MWSJ 9 na MWSJ 10 unaonyesha chanzo cha mila, kanuni zake na mchakato wa kuziadhimisha na kuzidumisha. Kwa mfano, ushairi wa MWSJ 6 unabainisha mila ya kutazama Mashariki wakati wa matambiko mbalimbali ya jando. MWSJ 10 inabainisha na kusisitiza kupitia kisasili cha chanzo cha jamii na mila ya Watachoni. Kuwa Misri. Ushairi huu vilevile umebainisha historia na maelezo ya njia na mahali walipopitia wakihama shughuli za jando walazojihusisha nazo pamoja na jamii walizotagusana nazo njiani mwao.

**Dhima ya Kuelimisha Jamii**

Kwa kutumia amali ya fasihi simulizi, wanajamii huelimishwa kuhusu thamani za kijamii, historia, utamaduni na mtazamo wao kilimwengu kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Kwa njia hii, jamii husika huhamasishwa juu ya mawazo yanayohusiana na tamaduni na desturi za jamii husika ili jamii hizo zipate mwelekeo unaowabainisha wao mbali na jamii zingine (Mwiza, 2014). Kulingana na Lihraw (2010), mawasiliano ya jando yalilenga kuwaelimisha watahiriwa na kuwafanya vijana kuwa wakamilifu machoni mwa mungu na kupata ufunguo wa kuingia ulimwengu huru na kuaminika kwa maarifa , maisha na mustakabali unaofaa katika jamii yao. Walifunzwa kuwa walikuwa wawakilishi wa jamii wakati huo na wakati wa jamii ujao ulikuwa mikononi, mwao. Katika mawasiliano haya ya jando, dhima ya kuwafunza vijana kuamini kuwa jando ilikuwa njia ya pekee kutimiza mahitaji ya tohara hii ya kiungu ilibainishwa. Vilevile, walihamasishwa watahiriwa kuwa watu kamili wanaotambua uwezo wao wa kuchangia ukuzaji, maendeleo na uhifadhi wa utamaduni wa jamii yao baadaye. Walifunzwa kujua kuwa utiifu wao kwa kanuni za jamii zao na zingine uliboresha uhusiano wao na Mungu. Uelewa huu uliwachochea watahiriwa kutilia



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing
Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

maanani kanuni hizo na kuzilinda kwa matumizi yake katika maisha yao baadaye.

Mawasiliano haya ya ushairi wa jando kama kipengele cha fasihi simulizi pia hulenga kutumika kama kinywa cha kutolea sheria, kanuni, maagizo na maelekezo yanayoiongoza jamii nzima katika kuendeleza shughuli zake za kila siku (Wanjala, 2015). Viongozi wa jando huwapa watahiriwa amali na mila za jamii kwa matumizi yao ya baadaye mathalani maadili, itikadi, matamanio na mihemko yao kwa kusifu na kukejeli watu wenye matukio mbalimbali yasiyofaa kama misingi ya kuwaelimisha watahiriwa na jamii kwa ujumla. Utafiti huu ulionyesha kuwa kila ushairi ulibeba mafunzo yaliyowalenga watahiriwa wa jando na jamii yao. Kwa mfano, ushairi MWSJ 1, uliwauliza Watachoni wa milango mbalimbali kufanyia shughuli zao pamoja kama jamii. Ushairi MWSJ 2 uliwahamasisha watahiriwa kuwa jasiri wanapofanya shughuli zao nao ushairi MMSJ 1, 2 na 3, watahiriwa wanauliza kulenga mbele jandoni kwa ujasiri ili kufaulu kupashwa jando na katika maisha yao ya baadaye. Hata hivyo, ilibainika kuwa baadhi ya wanaume Watachoni walikuwa wamesaidika sana maishani mwao kwa mafunzo hayo ya jando.

Watahiriwa wanapewa kanuni za kuwaelekeza katika maisha yao ya utu uzima ilivyo katika ushairi MWSJ 4 uliwataka wanajamii wafanye mila kwa kanuni za jamii yaani wa*cheze kwa mizizi ya mila*. Ushairi MWSJ 6 ulimhamasisha mtahiriwa kuhusu chanzo cha desturi ya kutazama Mashariki katika hatua mbalimbali za tohara ya jando. Ushairi MWSJ 9 ulimuelimisha kuhusu chimbuko la jamii ya Watachoni pamoja na namna mila hiyo inavyohusiana na jando. Ushairi MWSJ 10 uliakisi umuhimu wa sherehe ya kuwapitishia watahiriwa kwenye madhabahu ya *esitabicha* kama shule kuu ya kuwaandaa mahafali wa jando kwa kuwapa kanuni, kuwabariki na kuwakemea mahasidi wanaoweza kuzuka katika maisha yao ya baadaye. Shughuli na mawasiliano wanayoyapata katika ushairi huu iliwawezesha kuchukua mamlaka ya maisha yao ya baadaye kwa uhakika na ujasiri kama inavyosisitizwa katika nadharia ya Ubabe – dume iliyoongoza utafiti.

Mawasiliano ya ushairi wa jando vilevile yalilenga kuwaelimisha watahiriwa kuhusu lugha na mitindo inayotumika kuwasilisha ujumbe wa jando. Baadhi ya ushairi uliweza kubainisha chanzo cha misamiati tohozi ambayo imetumika. Hata hivyo, suala la utohozi wa msamiati kutoka kwa jamii zingine walizoathiriana nazo wakati wa uhamaji ulizua maswali zaidi ya majibu. Kwa mfano, iwapo Watachoni walikuwa na mila hii ya jando kule Misri, walitumia msamiati upi katika nafasi ya huu uliotoholewa njiani. Pia watahiriwa walielimishwa kuhusu maatumizi ya mitindo mbalimbali katika mawasiliano kama jazanda, taswira, maigizo, tashihisi, majigambo na mingineo.

**Dhima ya Kuburudisha**

Ushairi kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi huburudisha jamii kupitia vipera vyake vya fasihi vinavyolenga aghalabu kutumbuiza, kufurahisha na kusisimua. Wakati wa kuwapasha watahiriwa tohara ya jando huwa ni wakati wa kuburudika kwa wanajamii wote pamoja na majirani na marafiki wanaofika kushuhudia tohara hii. Vilevile, watahiriwa ambao huwa wamefanya



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

matayarisho kwa muda mrefu huburudika. Kwao, shughuli hii ya tohara ya jando huja mara moja tu katika maisha yao hivyo hubidi kuifurahia. Washiriki wote huburudika kwa kina kutokana na ushairi ulioimbwa mathalani nyiso na mahani ya tohara hii. Kulingana na Lihraw (2010), watahiriwa walipewa mafunzo kabla ya wakati huu kuhusu namna ya kucheza kengele kwa sauti na midundo ya kujifurahisha na kukidhi mahitaji mbalimbali ya jando.

Nyiso zinazowasilishwa hufanya hadhira kucheza kwa furaha kuathiri hali na tabia za mtahiriwa mkesha wa siku ya kuingia jandoni. Uimbaji wa ushairi huu na shughuli za jamii ya wachezaji hulenga kuwaburudisha watahiriwa na jamii ya Watachoni; kwa mfano, katika ushairi MWSJ 10 wa *Sankaya*, japo fanani ametumia mitindo ya hali ya juu kuwasilisha nyiso, mawasiliano yalichekesha zaidi ya kuelimisha na kuonya. Japo mawasiliano ya ushairi wa jando yaliwasilishwa kwa mahadhi na midundo maalumu ya kishairi iliyofurahisha na kuathiri nyoyo za watahiriwa na hadhira kwa jumla. Kila ushairi katika mitindo yake ya nyimbo au maghani uliwasilishwa kwa sauti zilizoburudisha masikio na kuathiri nyoyo za wote walioshiriki. Wasailiwa walikiri kuwa wakati wa mawasiliano haya jando katika hatua zote, watu wengi kutoka jamii zingine, watoto na hata wanahabari hufika kushuhudia na hata kunasa kwa vyombo vya kunasa sauti na picha kwa ajili ya kufurahia uwasilishaji wake. Hali hii ilidhibitisha kuwa mawasiliano haya hufurahisha kando na dhima zingine muhimu.

Kutokana na utafiti huu, ushairi mwingi ulibainika kuwasilisha ujumbe uliotiliwa mkazo kupitia mikarara yake. Zaidi ya kutilia mkazo ujumbe, mikarara hii pia ilibainika kuburudisha hadhira ya jando kutokana na kuleta midundo katika na kuyafanya mawasiliano haya kuburudisha. Kwa mfano, katika ushairi MWSJ 1, mkarara wake ulikuwa *Haahaa, Chapukeya* wenye kina cha nje ***ya*** kinachorudiwarudiwa katika ushairi wote. Ushairi MWSJ 4, *Eehehee, haahaa, ungeuliza...* Malumbano kati ya fanani na hadhira yalisababisha furaha kemkem katika mawasiliano ya jando. Maghani pia yaliburudisha hasa katika ushairi MMSJ 6 uliotumika kudhibiti tabia na mienendo ya wanajamii kuhakikisha maadili bora katika jamii. Kutokana na ushairi MWSJ 10, ilidhihirika namna waimbaji na wachezaji walivyokimbia, kupiga kemi na kupanda miti ili kukemea na kukejeli mabaya kwa njia iliyoburudisha Washiriki wanaume walidhihirika kuvalia mavazi ya kike na kucheza kwa mitindo ya kike kudhihirisha walivyoburudika. Washiriki wa mawasiliano haya walinengua maungo kudhihirisha walivyoufurahia shughuli hiyo. Matukio haya yote yalithibitisha raha waliyoipata waliohusika katika shughuli hizi za jando. Kilichoburudisha katika mawasiliano haya ya jando kilikuwa mitindo ya uwasiliashaji, lugha ya ucheshi na utani yenye mahadhi ya kishairi iliyotumika pamoja na uhusika wa fanani na hadhira walivyopokezana ujumbe kishairi. Sifa hizi ndizo zinazofanya mawasiliano haya kupendelewa japo yalikuwa na uchangamano katika kubainika kimaana iliyokusudiwa.

**Dhima ya Kukuza Sanaa na Ukwasi wa Lugha**

Mawasiliano ya ushairi wa jando hulenga kuitambulisha jamii, kueleza na kuhifadhi utamaduni wake kupitia mitindo na lugha ya uwasilishaji ujumbe. Kwa hivyo, watahiriwa hujifunza usanii hasa mitindo na sajili



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

mbalimbali ambayo huwaadilisha kuhusu matumizi yake kutegemea kaida na miiko katika jamii. Mawasiliano haya ya utanzu wa fasihi simulizi huchangia pakubwa ukuzaji ujuzi wa watumiaji wake na kusababisha ukwasi wa lugha hiyo hasa lugha ya Kitachoni inayosheheni mila muhimu za jando. Mitindo ya uwasilishaji ilizua walumbi wa mawasiliano ya jando waliodhihirisha ufundi mkubwa katika mitindo ya malumbano ya utani, hadithi, maghani, maigizo, mwingilianomatini na nyimbo za jando. Vilevile mitindo mbalimbali ya lugha iliyotumika kuwasilisha ujumbe katika ushairi huu mathalani jazanda, taswira, utohozi, takriri ililenga kuboresha sanaa na ukwasi wa lugha katika mawasiliano haya ya ushairi wa jando. Asemavyo Lihraw (2010), jando ilifungulia watahiriwa namna ya kuelewa wakati, kuweka hesabu ya matukio na kuhifadhi historia ya jamii yao. Watahiriwa waliweza kuzaliwa upya kutokana na mawasiliano haya na kupata hali mpya ya maarifa, matendo, ubunifu na uzalishaji.

Maghani katika ushairi MMSJ 1 yalidhihirisha usanii mkubwa wa kukemea mienendo mibaya katika jamii ya Watachoni. Kwa kuwarejelea walengwa wao bila kuwataja majina halisi kufidia utambulisho wao kupitia njia ya malumbano ya utani kati ya fanani na hadhira huku wakitoa ujumbe uliokuwa na mafunzo muhimu kwa watahiriwa na jamii kwa ujumla. Watahiriwa walibaini namna ya kuwakosoa wakosaji kwa njia isiyo ya moja kwa moja kama ilivyodhihirika kuwa waliolengwa kwa mawasiliano haya. Mawasiliano haya yalilenga kudhihirisha namna mawasiliano ya ushairi huu hukuza lugha husika baada ya kuelewa maana inavyotumika katika miktadha yake inavyoelekezwa kwa nadharia ya Baada ya Umuundo. Kwa mfano matini ya ushairi MMJS 6 yamedhihirisha ukwasi wa lugha na sanaa ya maigizo ambayo yalikuza lugha ya walengwa mno.

Mawasiliano haya ya ushairi wa jando vilevile yalitumiwa kukuza lugha ya Watachoni kwa kutumia maneno toholevu kutoka lugha nyingine ambazo pia huwa na tohara kama hii. Aghalabu maneno haya huweza kueleweka tu katika muktadha wa jando kama vile: Esitabicha (MMSJ 5), Sankaya/ sangaria/ sangaya (MWSJ 10), Cheputalang'/ Cheputalal (MWSJ 9), Merinde/Merindo (MWSJ 9), Avilikwemboi (MWSJ 7), Aejelayo (MWSJ 7), Ekakuyeche (MWSJ7) na mengine. Haya maneno yalichangia ukuzaji wa lugha katika mawasiliano haya ya ushairi wa jando kwa njia ya utohozi. Viongozi walipoyatumia katika nyimbo na ushauri, watahiriwa walijifunza na kujiendeleza katika matumizi ya lugha na ilichangia kuziendeleza mila na desturi za Watachoni. Hata hivyo, Bryan (1959) akimnukuu Huntingford (1968) alitahadharisha dhidi ya kutumia lugha kubainisha uhusiano wa jamii tofauti kwani haikuwezekana kuwa na zaidi ya lugha mbili mame ila pengine lugha hizo ziliweza kuingia katika kizazi cha jamii kwa wakati tofauti. Naye Lihraw (2010) alituthibitishia kuwa Watachoni walikutana na Wakalenjin kwa mara ya kwanza Torit katika Sudani ya kusini na kuingia nao nchini Kenya kupitia Sirikwa kama Wakitoki na Wakalenjin. Kwa hivyo, maelezo haya yalifanya tuelewe utohozi mwingi ulitokana na lugha za Kikalenjin.

**Dhima ya Kuitambulisha Jamii**

Jamii huweza kutambulika kupitia utamaduni wake ambao huelezwa vyema zaidi kupitia fasihi simulizi mathalani nyimbo, ngano na maghani (M'Ngaruthi,



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

2008). Kila jamii huwa na mitindo yake ya kuwasilisha sanaa za fasihi ambayo huwa kitambulisho chake. Vilevile, visasili, mivigha na nyimbo mbalimbali huwa kati ya vipengele vinavyoitambulisha jamii husika. Lugha inayotumiwa hutambulisha jamii na kudhihirisha uhusiano wa kitamaduni uliopo kati ya wanajamii wake. Jamii husifika kutokana na sanaa yao katika fasihi simulizi kama vile ushairi. Miktadha ya kitamaduni na kihistoria huongoza uteuzi wa lugha kwa msanii yeyote, kwani lugha husheheni mila, itikadi, amali, tabia na mawasiliano ya jamii husika (Wanjala, 2015). Mawasiliano ya ushairi wa jando hutambulisha utamaduni wa Watachoni namna unavyofanywa katika awamu mbalimbali za jando. Kwa mfano, katika ushairi MWSJ 1, koo mbalimbali zilibainishwa kulingana na jinsi zinavyojitambulisha kwa sehemu walizopitia, kuishi na shughuli walizofanya. Ushairi huu uliwahimiza wanajamii kushirikiana hasa katika ushairi MWSJ 1 *Chapukeywa* iliyomaanisha kufanyia pamoja. Ushairi huu pia uliwahimiza Watachoni kushikilia mila ili kuiendeleza kwa pamoja. Vilevile ulitambulisha milango mbalimbali ya Watachoni na namna ya wanavyojitambulisha kama sehemu ya jamii pana. Uliwahamasisha Watachoni waweze kusherehekee mila yao na kuiendeleza kwa pamoja na furaha.

Matokeo ya Utafiti huu ulidhihirisha kuwa mila ya jando huitambulisha jamii ya Watachoni. Ushairi MMSJ 3 ulidhihirisha namna mila hii ya jando ilikuwa imetekelezwa na Watachoni kwa miaka mingi bila wao kuogopa. Utambulisho wa jamii ya Watachoni ilisisitizwa sana kwa matumizi ya usemi *sisi hatuogopi kamwe kisu cha ngariba.* Kulingana na babu, jamii ya Watachoni inatambulikana kutokana na ujasiri wao katika tohara ya jando. Ushairi MWSJ 5 unasisitiza utambulisho huu fanani anaposema kuwa *wanaopiga nduru kuwa si tabia yao (Watachoni)* na *wanaoogopa waende Ujaluoni katika.* Kwa hivyo, watu waoga hawawezi kujitambulisha kuwa Watachoni ila walioimudu jando kwa ujasiri pekee yao. Ushairi MWSJ 8, unadhihirisha kuwa mwanamume Mtachoni hutambulikana kutokana na kupashwa jando. Watachoni wasiotahiriwa hawakupewa majukumu ya watu wazima na walipofariki, ilikuwa lazima watahiriwe kabla ya kuzikwa. Watahiriwa wengi walibainisha dhima hii na ikawa jambo lililowachochea kukabiliana na tohara hii kishujaa.

Utafiti huu ulibainisha kupitia ushairi MWSJ 6 kuwa Watachoni huitambulishwa kwa misingi ya mahali walipotoka (Chimbuko), sehemu walizozipitia wakihama na shughuli za kimila walizozifanya njiani wakihamia makazi yao ya sasa. Ushairi huu uliwatambulisha Watachoni kutokana na ulivyosemwa kuwa wao wa *Kiboriti walitoka Mashariki.* Vilevile, mila yao ilisemekana kuwa ilitoka Mashariki hali ambayo ilitumika kueleza sababu za wao kutazama Mashariki wanapofanya mila zao za jando kama vile kuwekea mtahiriwa nyama shingoni, kupakwa tope, kutahiriwa na kadhalika. Kila jamii huwa na ushairi wake hasa nyimbo ambao huzitumia nyakati za kuwaingiza au kuwatoa watahiriwa jandoni. Utafiti huu ulithibitisha kuwa *ekakuyeche* ndio ushairi unaoimbiwa mtahiriwa anapowekewa nyama shingoni, anaporuhusiwa kuanza kuwaalika jamaa na marafiki katika jando na anapotolewa mtoni siku ya kutahiri. Kando na ushairi huu kulenga kumtia mori wa kukikabili kisu, hubainisha kuwa mtahiriwa ni Mtachoni. Kwa hivyo, dhima kuu ya mawasiliano ya ushairi wa jando kutokana



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

na matokeo ya utafiti huwa kitambulisho cha mila ya Watachoni.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### Hitimisho

Kutokana na uchambuzi tulioufanya katika utafiti huu kuhusu mawasiliano ya ushairi wa jando katika jamii ya Watachoni, ilidhihirika kuwa ushairi huu hutekeleza majukumu muhimu katika kuwaandaa watahiriwa kwa maisha yao ya baada ya jando. Maandalizi haya hulenga kuwapa uwezo wa maarifa na mamlaka ya kutekeleza majukumu yao ya kijamii na kuendeleza uhifadhi wa utamaduni na historia ya jamii ya Watachoni.

Utafiti huu ulibainisha kuwa mawasiliano ya ushairi wa jando huwa na dhima muhimu katika jamii ya Watachoni wa Kaunti ya Bungoma. Ilipatikana kuwa umuhimu wa pekee ulipashwa mtahiriwa kulingana na majukumu ya yake utu uzima ya kuwa mwanamume, baba, kiongozi wa kijamii kupitia kubalehe kutokana na mafunzo ya jando. Dhima za mawasiliano haya zilizoainishwa katika utafiti huu zilikuwa kudumisha utamaduni na kuendeleza historia, kuelimisha, kuunganisha jamii, kuburudisha, kuitambulisha jamii, kukuza maadili pamoja na kukuza sanaa na ukwasi wa lugha kwenye jamii ya Watachoni. Ilibainika kuwa mawasiliano haya hulenga kuwatoa wavulana Watachoni kutoka katika maisha ya kitoto hadi utu uzima ili wajukumike kuendeleza dhima za jando namna zilivyodhihirika kutokana na utafiti huu. Dhima katika mawasiliano haya zilitokana na mitindo mbalimbali ya uwasilishaji mathalani nyimbo na maghani iliyosheheni mafunzo kwa watahiriwa na jamii ya Watachoni kwa jumla.

### Mapendekezo

Vilevile, ilibainika kuwa asilimia nzuri wana shida ya kupata na kutumia mafunzo yanayotolewa kupitia mawasiliano ya ushairi wa jando. Utafiti huu umependekeza kuandaliwe warsha ya kuwahamasisha mahafali wa jando juu ya mafunzo muhimu kuhusu masuala ya upashaji jando katika jamii ya Watachoni kila baada ya miaka minne.

Viongozi wanaohusikana na mawasiliano ya ushairi wa jando wapitishiwe katika semina ya kuwaboresha katika uteuzi wa matini na mitindo mwafaka ya uwasilishaji wa mawasiliano ya ushairi wa jando katika jamii ya Watachoni.

## MAREJELEO YA KIMSINGI

Abu-Lughod, L. (1986). *Veiled Sentiments*. Berkeley: University of California Press.

Alembi, E. (1991). *Don't be Long John*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Bryan, M.A. (1959). T/K Language in East Africa, 29(1) Pp.1

Coplan, D. (1987). Eloquent Knowledge: Lesotho Migrants' songs and the Anthropological Experience. *American Anthropologist*, 14(3), 413-33.

Derrida, J. (1966). "Structure, Sign, and Play in the Discourse of Human Science" and Presented



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 07.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Iyaya, R. M., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Gills, J. &Waters, M. (2014). Poetry and Autobiography in the Journal Life Writing, 6 (1).

Huntingford, C.W.B. (1968). *History of East Africa. Vol. 1*
in the Languages of Criticism and Science of Man in 1967.

Leane, E. (2015). *Antarctica in Fiction:* Imaginative Narrative of the Far South. Cambridge University Press.

Lihraw, D. O (2010). *The Tachoni Peoples*: *History, Culture and Economy*. Entrepreneurship Development Institute (EDS), Nairobi.

M'Ngaruthi, T. N. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*: Kitabu cha Walimu na Wanafunzi (Shule na Vyuo). The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Maclennes, J. (1998). *The End of Masculinity*. Buchingham Open University Press.
*Mashairi ya Shabaan Robert. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria,*

Momanyi, C. (2007). Patriarchal Symbolic Order. The Syllables of PowerAccentiated in Waswahili Poetry. *The Journal of Pan African Studies*, 1(8).

Musira, W. (2015). *Utanzu wa Fasihi Simulizi.* Makala katika Swahilihub.com.

Mwiza, P. (2014). Umuhimu wa Fasihi Simulizi katika jamii. Kutoka *petermwiza Blogspot.com*
*na Mwaka wa Kogwa.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Salem, B. M. (2013). *Usawiri wa Jinsia Katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka katika Tanzania.*

Truswell, R. & Gisborne, N. (2014). Quantificational Variability and the Genesis of English Headed Wh-relatives. In the Proceedings of Sinn and Bedeutung 19. Edinburgh University.

Wanjala, F. S. (2015). Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa *Embalu*



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org